Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

# JARIDA la Mtandaoni la NSSF

## TOLEO LA JULAI 2024 - NSSF ILIVYOTOA HUDUMA SABASABA



Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

**NSSF**

Simu Bure 0800116773

@NssfTanzania

# MSHOMBA AFICHUA SIRI MAFANIKIO YA NSSF

## Asema mazingira mazuri ya uwekezaji chini ya uongozi wa Mhe. Rais Dkt. Samia yamechochea mafanikio



**Na MWANDISHI WETU**

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Bw. Masha Mshomba amefichua siri ya mafanikio makubwa ambayo NSSF imeyapata kuwa yamechangiwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyohamasisha wawekezaji katika sekta binafsi, kuweka mazingira mazuri na kuwezesha kupata waajiri na wanachama wengi wapya katika sekta binafsi.

Bw. Mshomba alisema hayo tarehe 3 Julai, 2024 wakati alipotembelea banda la NSSF mara baada ya ufunguzi wa Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF) maarufu SabaSaba yaliyobeba kauli mbiu isemayo "Tanzania Sehemu Sahihi kwa Biashara na Uwekezaji." Maonesho hayo yalifunguliwa na Mhe. Filipe Nyusi, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji akisindikizwa na mwenyeji wake, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Akizungumza na waandishi wa habari katika banda la NSSF, Bw. Mshomba alisema kwa mujibu wa taarifa za hesabu ambazo hazijakaguliwa katika mwaka wa fedha 2023/2024, thamani ya NSSF kwa sasa inafikia trilioni 8.5 sawa na ongezeko la asilimia 77% ukilinganisha na miaka mitatu iliyopita.

"Ongezeko hili ni kubwa hasa ukizingatia kuwa ndani ya miaka mitatu iliyopita ukuaji wa NSSF umekuwa mkubwa mno, hivyo tunampongeza sana Mhe. Rais Dkt. Samia kwa juhudi anazoweka katika kuhakikisha mazingira ya biashara hapa nchini yanakuwa mazuri ambayo yamechangia mafanikio haya," alisema Bw. Mshomba.

Alisema wakati NSSF inaendelea kutekeleza mpango wake wa maendeleo unaoishia Juni 30, 2026, wanatarajia thamani ya Mfuko kufikia trilioni 11 ambayo itakuwa ni zaidi ya mara mbili ukilinganisha na kipindi ambacho Rais Dkt. Samia alipoingia madarakani.

Bw. Mshomba alisema kwa sasa NSSF imeelekeza nguvu ya kuwafikia wanachama wapya waliopo katika sekta isiyo rasmi ili waweze kujiunga na kuchangia katika NSSF kwani tayari wameshaweka mifumo mizuri ya usajili na uchangiaji pamoja na mafao yanayovutia kupitia Mpango wa Kitaifa wa Sekta Isiyo Rasmi.

Alisema ushiriki wa NSSF katika maonesho hayo ni kwa ajili ya kutoa elimu ya hifadhi ya jamii kwa wanachama na wadau kuhusu huduma mbalimbali ambazo NSSF unazitoa zikiwemo usajili wanachama kutoka sekta binafsi na sekra isiyo rasmi, uchangiaji, kulipa mafao, uwekezaji pamoja na uhakiki wa wastaafu.

Bw. Mshomba alisema pia wanatumia maonesho hayo kuwaeleza wanachama mambo makubwa ambayo NSSF imeyafanya kupitia huduma za TEHAMA ambapo sasa wanachama wanaweza kujisajili kupitia lango la huduma binafsi kwa mwanachama (Member Portal) na lango binafsi kwa mwajiri (Employer Portal).

Alisema NSSF inaendelea kupata ushirikiano mkubwa kutoka Serikalini hivyo wataendelea kuboresha huduma zao mbalimbali.

# JK KATIKA BANDA LA NSSF

**Na MWANDISHI WETU**

Rais Mstaafu wa awamu ya nne, Mhe. Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alitembelea banda la NSSF na kupata maelezo kutoka kwa Bi. Lulu Mengele, Meneja Uhusiano na Elimu kwa Umma, kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Bw. Masha Mshomba.

Bi. Lulu alimueleza Mhe. Dkt. Kikwete kuwa NSSF inatoa elimu ya hifadhi ya jamii kwa sekta binafsi na sekta isiyo rasmi, kuandikisha wanachama wapya katika sekta isiyo rasmi ambao wanachangia kuanzia shilingi 30,000 kwa mwezi kwa ajili ya kujiwekea akiba yao ya sasa na ya baadaye.

Naye, Meneja wa Sekta isiyo rasmi, Bi. Rehema Chuma alimueleza Rais Mstaafu Mhe. Dkt. Kikwete kuwa NSSF imetanua wigo na kuifikia sekta isiyo rasmi ambapo wanapata mafao yote na uchangiaji wake ni rahisi kupitia kumbukumbu namba ya malipo ya Serikali (Control number) kwa njia ya simu au benki.




# NSSF YAWATAKA TWCC KUCHANGAMKIA FURSA YA KUJIUNGA NA KUJIWEKEA AKIBA

Meneja wa Sekta isiyo rasmi wa NSSF, Bi. Rehema Chuma akiwa na wafanyakazi wengine wa NSSF, walitembelea banda la Chemba ya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC), na kutoa elimu ya hifadhi ya jamii kwa wanachama wa Chemba hiyo walioshiriki Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), ambapo aliwaeleza umuhimu wa kujiwekea akiba kwa kujiunga na kuchangia NSSF ambapo kwa mwezi watachangia kiasi cha shilingi 30,000 kima cha Chini.











# HABARI PICHA

Wananchi waliotembelea banda la NSSF wakinufaika na huduma mbalimbali zilizokuwa zinatolewa katika banda la NSSF zikiwemo elimu ya hifadhi ya jamii, usajili wa wananchi walio katika sekta isiyo rasmi, mifumo ya TEHAMA, mapambano dhidi ya rushwa, miradi ya uwekezaji na huduma za NSSF kidijitali
















# NSSF NDANI YA BANDA LA OFISI YA WAZIRI MKUU SABASABA 2024

**Na MWANDISHI WETU**

Wafanyakazi wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Lucas Laizer na Rehema Msumi wakitoa huduma kwa wateja waliotembelea banda la Ofisi ya Waziri Mkuu na Taasisi zake. NSSF ilishiriki katika Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), SabaSaba. Kupitia Maonesho hayo, NSSF ilitoa elimu ya hifadhi ya jamii, usajili wa wananchi walio katika sekta isiyo rasmi, mifumo ya TEHAMA, miradi ya uwekezaji na huduma za NSSF kidijitali.






# NSSF YATWAA TUZO MAONESHO YA SABASABA

**Na MWANDISHI WETU**

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umetwaa tuzo ya mshindi wa pili, kundi la sekta ya Hifadhi ya Jamii na Bima, kwenye kilele cha Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF). Tuzo hiyo ilipokelewa na Meneja wa Sekta Isiyo Rasmi wa NSSF, Bi. Rehema Chuma kutoka kwa Dkt. Aboud Suleiman Jumbe, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Maonesho ya SabaSaba mwaka huu yalifungwa rasmi na Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tarehe 13 Julai, 2024.




# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA









BOARD OF TRUSTEES
NSSF
NATIONAL SOCIAL SECURITY FUND
Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye
Miliki Nyumba ya ndoto yako
estate.salesmarketing@nssf.go.tz
0756 462 267, 0682 110 634
KIJICHI, DUNGU, TOANGOMA
@NssfTanzania
www.nssf.go.tz

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF),
Jengo la Benjamin William Mkapa, Mtaa wa Azikiwe
S.L.P 1322, Dar es Salaam, Tanzania

**Simu Bure: 0800116773,**
**Barua pepe: customercare@nssf.go.tz**
**Tovuti: www.nssf.go.tz**